MATUNDASI ASM DEVELOPMENT COMPANY LIMITED
https://www.matundasiasm.co.tz/ info@matundasiasm.co.tz

**28 Mei, 2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Matundasi ASM Development Company Limited (MADC) ni kampuni inayojishughulisha na utafiti na uchimbaji wa madini katika Mkoa wa Mbeya, wilaya ya Chunya. Kampuni hii inawatangazia wote wenye sifa tajwa kuwasilisha maombi ya kuajiriwa katika nafasi mbalimbali kama ifuatavyo:

## MADEREVA WA MALORI (Truck Drivers)

**DEREVA WA MALORI DARAJA LA I (Truck Driver I) –** Nafasi mbili (02)

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Cheti cha kidato cha nne.
- Awe na cheti cha VETA au Diploma ya Udereva.
- Leseni halali ya udereva (Daraja E) kutoka chuo cha udereva kinayotambulika.
- Uzoefu usiopungua miaka 7 katika udereva wa malori.
- Uelewa wa matengenezo na utambuzi wa matatizo ya mitambo.
- Uelewa wa sheria za barabarani na alama za barabarani za Tanzania na nchi jirani.
- Cheti cha kozi ya udereva wa kujihami (defensive driving course) kutoka LATRA kitahesabiwa kama sifa ya ziada
- Uwezo wa kuwasiliana vizuri na wasimamizi.
- Uwezo wa kufuata ratiba za usafirishaji zilizopangwa.
- Uwezo wa kuendesha malori yenye tela au vifaa maalum.
- Uwezo wa kujaza daftari la safari, na fomu za ukaguzi wa gari.
- Umri usiozidi miaka 45.

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:**

- Maombi yaelekezwe kwa:
  **Afisa Rasilimali Watu**
  Matundasi ASM Development Company Limited,
  S.L.P 70812,
  DAR ES SALAAM,
- Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe info@matundasiasm.co.tz na hr@matundasiasm.co.tz
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20 Juni, 2025,** na kichwa cha barua pepe kiwe jina la nafasi unayoomba.

**VIAMBATANISHO MUHIMU**

- Waombaji wenye sifa wanatakiwa kuwasilisha barua ya maombi ikiwa na nyaraka zifuatazo:
  a) Nakala za vyeti husika (vilivyothibitishwa),
  b) Nakala ya leseni
  c) Nakala ya cheti Cha utumishi (kampuni aliyotoka)
  d) Picha mbili (2) za pasipoti za hivi karibuni,
  e) Wasifu binafsi (CV)
  f) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
  g) Police Fingerprint.
  h) Wadhamini watatu (wa nje na ndani ya familia ikiwa na picha za wadhamini na anuani zao (nambari za simu)
  i) Barua ya wadhamini watatu, mmoja (01) wa nje na wawili (02) wa familia pamoja na picha(passport) zao na mawasiliano yao yanayopatikana.
  j) Barua ya utambulisho kutoka serikali za mtaa anapotokea.
- Waombaji waliotimiza vigezo ndio watakaoitwa kwa ajili ya usaili.

MATUNDASI ASM COMPANY LTD